**HUDUMA ZA WAKALIMANI ZINAPATIAKNA BILA MALIPO**

Tafadhali tuarifu kama unahitaji mkalimani au msaada mwingine ili uweze kusoma na kuelewa ilani hii.

**ILANI HII INAKUARIFU JINSI TAARIFA ZA TIBA, NA TAARIFA ZINGINE ZINAZOKUHUSU ZINVYOWEZA KUTUMIWA NA JINSI UNAVYOWEZA KUZIPTA.**

**TAFADHALI KAGUA KWA MAKINI**

Taarifa ya Afya Mazoea ya Faragha: **Ukurasa 1-3**

Mazoea ya Jumla Kuhusu Habari Binafsi tambulishi: **Ukurasa 4**

"Sisi" ni Wakala wa Huduma ya Jamii (AHS). AHS inajumuisha Idara ya watoto na familia; Idara ya Walemavu, Wazee wanaoishi wenyewe; Idara ya afya; Idara ya afya ya akili; Idara ya magereza; na Idara ya huduma za afya ya Vermont. Wakandarasi na wafadhili wetu ni pamoja na watoa huduma za jamii katika Vermont, kama vile vituo vya wazazi na watoto, vituo vya watu wazima, na vituo vya wagonjwa wa akili.

Tunapokupatia huduma za afya na kijamii, tutachukua habari zinazokutambulisha binafsi (habari za kutambulisha), na wakati mwingine habari juu ya afya yako. Inatulazimu kuhifadhi maelezo haya chini ya sheria ya Serikali Kuu na ya Jimbo, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Bima ya Afya ya Shirikisho na Uwajibikaji wa sheria ya 1996 inayojulikana kama HIPAA ("Sheria ya faragha") .

Notisi hii inakueleza jinsi gani tunaweza kutumia au kutoa kwa wengine taarifa yako binafsi na/au maelezo yako ya afya na wakati gani hatuwezi kufanya hivyo. Pia inakuarifu juu ya haki zako. Kisheria tunatakiwa kukupa notisi hii. Sheria pia inatutaka kufuata maadili ya notisi hii kama yalivyopitishwa kwa wakati huu.

## KUHUSU USIRI WA HUDUMA UNAZOPATA: HABARI ZA KIAFYA

### 1. AHS ina habari gani za afya kuhusu mimi?

Wewe na wengineo mnaweza kutupatia maelezo kuhusu afya yenu na huduma za afya unapoomba au kupata huduma zetu. Hii inaweza kuwa pamoja na maelezo kuhusu ugonjwa ulionao, ulemavu au matibabu unayopata. Hii inaweza pia kuwa pamoja na maelezo ya kifedha.

### 2. AHS inatumia na kutoa kwa wengine habari gani za kiafya?

Tunatumia na kutoa kwa wengine habari za afya zilizo na umuhimu tu kwa wafanya kazi wetu na wakandarasi kwa ajili ya kutimiza kazi zao.

### 3. AHS inatumia na kutoa kwa wengine maelezo yangu ya kiafya wakati gani?

Tunaweza kutumia na kutoa kwa wengine maelezo yako ya kiafya kwa ajili ya tiba, malipo, au katika kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na mpango wa kutoa huduma na shughuli za utawala za AHS. Kwa mfano, tunaweza kutumia maelezo yako kwa sababu zifuatazo:

- Kutambua kama unawajibika kupata huduma na msaada wetu.
- Kuanzisha na kutoa mpango maalum wa huduma au matibabu.

*Kwa mfano, tunaweza kutoa kwa wengine maelezo yako kwa ajili ya kufanya mpango wa matibabu na manesi, madaktari na wafanyakazi wengine wa afya wanaokutibu.*

- Kukukumbusha katika kupanga tarehe za kukutana na madaktari.

- Kukuarifu kuhusu huduma nyingine na misaada mengine iliyopo au matibabu ambayo yanaweza kukusaidia wewe au familia yako.
- Kufanya malipo kwa huduma zako.

*Kwa mfano,daktari wako anaweza kutuletea maelezo yako ya kiafya ili tuweze kumlipa. Tunaweza pia kutoa habari zako za afya kwa wakandarasi wetu ili wawezi kumlipa daktari wako kwa niaba yetu.*

- Kuweza kufanya kazi zetu na kuendeleza mipango yetu

*Kwa mfano, tunaweza kutumia na kutoa kwa wengine maelezo yako ya kiafya kuhakikisha kuwa watu wanaokuangalia wanakupa huduma zilizo bora na za hali ya juu na wanalipwa bila kuchelewa na inavyotakiwa. Tunaweza kutumia na kutoa kwa wengine maelezo yako kuhakisha kuwa unapata huduma kamilifu na kuweza kuboresha huduma unazopata.*

**4. Je, kuna wakati ambapo AHS inatumia na kutoa habari zangu za kiafya kwa wengine bila ya idhini yangu?**

Ni mara chache ambapo tunatumia na kutoa habari zako kwa wengine bila ya idhini yako. Wakati mwingine sheria inaturuhusu au inatutaka tufanye hivyo.

Tunaweza kutoa habari zako kwa wengine bila ya idhini yako kwa sababu binafsi zifuatazo:

- Na ndugu/jamaa zako au mtu mwingine uliyemchagua, kuhusiana na kuhusika kwao katika kukuangalia au malipo kwa ajili ya tiba yako.
- Kuarifu familia yako au mtu mwingine anayehusika katika tiba yako kuhusiana na mahala ulipo, hali yako au kifo.
- Kwa mkurugenzi wa maswala ya mazishi au mchunguzi wa afya kumpatia habari ili wafanye kazi yao mtu anapo fariki.
- Kwa fidia yako ya kikazi au malipo mengine ya namna hiyo.

Tunaweza kutoa habari zako kwa wengine bila ya idhini yako kwa sababu maalum zifuatazo:

- Kwa shughuli za afya ya umma kama vile kukinga au kudhibiti magonjwa, Kusaidia kutoa taarifa ya kurejeshwa bidhaa mbovu, kutoa taarifa juu ya madhara ya dawa., kuumia au
- Kwa ajili ya utafiti, tukizingatia sheria kali zilizowekwa
- Na mashirika yanayohusika na kutoa sehemu za mwili zilizohifadhiwa kwa ajili ya kusaidia wanaohitaji.
- Katika kuitikia mwito wa korti au serikali, kuhitajika kortini, maombi katika uchunguzi, au kwa shughuli nyingine za namna hiyo.
- Kwa polisi kama itahitajika kisheria
- Kuripoti uhalifu uliofanyika katika maeneo yetu au kwa wafanyakazi wetu.
- Kuripoti unyanyasaji, uzembe, au uonevu kijamii kwa mamlaka zinazohusika.
- Kwa shirika la usimamizi wa afya, kwa ajili ya shughuli zilizoruhusiwa kisheria kama vile ukaguzi na uchunguzi.
- Kwa Idara ya Afya na Huduma ya Jamii ya Marekani katika kuangalia kama inafuata maadili au kufanya uchunguzi wa malalamiko.
- Kuepusha kusitokee madhara ya kiafya au usalama wa mtu au umma, au afisa usalama kwa kusudi la usalama.
- Kufanya kazi maalum za kiserikali, kama vile kulinda maafisa wa umma, kwa usalama wa taifa, kwa maswala ya kijeshi, na kwa magereza kwa sababu fulani fulani.
- Na wazimamizi wa wakala wa afya kwa ajili ya shughuli zilizoruhusiwa kisheria
- Na wakala mwingine anayesimamia programu ya serikali inayotoa mafao ya umma, kuhusiana na taarifa za kustahiki au uandikishaji, na kuratibu vyema, kusimamia na kuendesha mipango inayohusiana na serikali.

  Isipokuwa kwa sababu zilizoainishwa katika ilani hii, au vinginevyo kuruhusiwa kisheria, hatutatumia au kutoa habari zako za kiafya bila idhini yako kwa maandishi..

**5. Je! Ikiwa mtu mwingine anahitaji habari yangu ya kiafya?**

Unaweza kutueleza kama unataka tutoe maelezo yako kwingine au tunaweza sisi kutaka ruhusa yako ili tuweze kufanya hivyo. Kabla hatujatoa maelezo yako yoyote kwingine, utaombwa kutia saini kwenye fomu maalum ya kutoa ruhusa hiyo. Fomu hiyo ya ruhusa inatueleza habari gani tunaweza kutoa, sababu ya kutoa habari hizo, na maelezo ya

mtu/watu ambao habari hizo zinatolewa kwao. Unaweza kufuta ruhusa hiyo wakati wowote.

### 6. Je, Ninaweza kuchagua mtu wakuniwakilisha?

Ikiwa umempa mtu nguvu ya wakili wa matibabu au ikiwa mtu ni mlezi wako wa kisheria, mtu huyo anaweza kutumia haki yako na kufanya uchaguzi juu ya habari yako ya afya. Tutahakikisha mtu huyo ana mamlaka hii na anaweza kukuwakilisha kabla ya kuchukua hatua yoyote.

### 7. Je, Naweza kuona taarifa zangu za afya?

Kwa ujumla, unaweza kuona habari yako ya afya. Unapaswa kumwuliza Afisa wa Faragha, kwa maandishi, kuiona au kupata nakala yako (tazama habari ya mawasiliano kwenye ukurasa wa 3) Tutatoa nakala au muhtasari wa taarifa za afya yako na madai, kwenye siku 30 za ombi lako.4). Unaweza pia kuomba nakala za elektroniki za habari ambazo tunashikilia kwa njia ya elektroniki. Usalama au sababu zingine za kisheria zinaweza kupunguza habari unayoona. Tunaweza kutoza kiasi linganifu kwa kunakili.

### 8. Ninaweza kubadilisha maelezo yangu ya afya?

Kama unafikiri kuna maelezo ya afya ambayo si sahihi katika rekodi zetu unaweza kutuandikia ili tufanye marekebisho au tuongeze maelezo mapya. Unaweza kuomba tupeleke maelezo hayo yaliyorekebishwa au maelezo mapya kwa wengine ambao wamepata maelezo yako kutoka kwetu.

Kama kwa maoni yetu tunaona kuwa maelezo yako ni sahihi na kamilifu, au kwa sababu nyingine, hatutakuwa na haja ya kufanya mabadiliko au kuongeza maelezo yeyote. Kama hatukubali kubadilisha maelezo yako, tutakuambia, kwa maandishi, ndani ya siku 60, kwa nini hatukubali. Pia tutanakili katika rekodi zetu kwamba umetutaka tubadilishe maelezo yako na kwamba hatukukubali kuyabadilisha.

### 9. Je ninaweza kuiomba AHS iweke masharti namna inavyotumia na kutoa maelezo yangu ya afya kwa wengine?

Unaweza kuomba tuweke masharti namna tunavyotumia na kutoa maelezo yako kwa wengine. Maombi yako yanatakiwa yawe ya maandishi na utueleze unataka masharti gani. Tutalifikiria ombi lako lakini hatulazimiki kulikubali.

### 10. Je, Naweza kuiomba AHS iwasiliane na Mimi kwa njia ya siri?

Unaweza kuomba kwamba tunawasiliana nawe kwa njia mbadala inayofaa au katika eneo lingine. Ombi lako lazima liwe katika maandishi na utuambie ni wapi na jinsi tuapaswa kuwasiliana nawe. Tutajaribu kuheshimu ombi lako

### 11. Je ninaweza kupata orodha ya lini AHS imetoa habari zangu za afya kwa wengine?

Unaweza kuomba upatiwe orodha ya maelezo yako yaliyotolew kwa wengine. Unatakiwa utume maombi yako kwa maandishi kwa afisa wa maswala nyeti. Sheria haitulazimu tuodhoreshe matukio yote yaliyotufanya tutoe maelezo yako kwa wengine. Kwa mfano, hatuna ulazima wa kuorodhesha wakati tulipotoa maelezo yako kwa wengine kwa matibabu ya AHS, malipo au utoaji wa huduma za afya, au tulipoltoa maelezo yako kufuata na idhini uliyoitia na kutia saini.

### 12. Je, nitajulishwa ikiwa kutakuwa na ufichuzi wa faragha au usalama wa taarifa yangu ya afya?

Tutakujulisha kwa barua ikiwa kutakuwa na ufichuzi wa taarifa ya ya afya. Ufichuzi hutokea wakati mtu anaona, anatumia au anafichua taarifa ya afya iliyolindwa bila ruhusa kwa namna inayohatarisha faragha na usalama wa taarifa ya afya.

### 13. Sheria gani AHS inafuata ambayo inahusiana na hifadhi ya maelezo yangu ya afya?

Tunafuata sheria ya serikali kuu ya Sheria ya Bima ya afya ya mwaka 1996 (Health Insurance Portability and Accountability Act of 1996), ijulikanayo kama HIPAA. Pia tunafuata sheria yoyote ya serikali kuu au ya jimbo ambayo inakinga zaidi kuliko HIPAA, popote inapowajibika. Kwa mfano, tunafuata sheria ya hifadhi ya serikali kuu kuhusiana na mipango ya matibabu kutokana na matumizi mabaya ya dawa za kulevya, 42 CFR s ehemu ya 2, na ya jimbo katika rekodi za tiba ya akili, 18 VSA § 7103.

### 14. Je, ninaweza kupata nakala ya notisi hii?

Ndiyo, unahaki ya kupata nakala ya notisi hii. Unaweza kutuomba nakala wakati wowote. Nakala kwa njia ya mtandao inapatikana katika tovuti yetu ya, www.humanservices.vermont.gov.

## 15. Je, AHS inaweza kubadilisha usiri wa huduma zake?

Tuna haki ya kubadilisha usiri wa huduma zetu na notisi hii. Mabadiliko yoyote katika kazi yetu yatafanyika katika maelezo kuhusu wewe ambayo tunayo tayari na maelezo ambayo tutapata kwa siku zijazo. Tutatuma nakala ya notisi mpya katika tovuti yetu www.humanservices.vermont.gov, na kukupatia nakala kwa njia ya posta.

### 16. Je nitawasiliana na nani kama nina swala kuhusu notisi hii?

Tafadhali wasiliana na afisa wa maswala nyeti **Privacy Officer** kwa simu namba 802-241-0225 au kwa njia ya posta:
AHS Privacy Officer
c/o Agency of Human Services
Office of the Secretary
280 State Drive Center Building
Waterbury VT 05671-1000

### 17. Nitalalamika vipi kama ninaamini kuwa haki yangu ya hifadhi imekiukwa?

Unaweza kutuma malalamiko yako kwa afisa wetu wa maswala nyeti kwa barua au simu. Unaweza pia kutoa malalamiko kwa afisa wa haki za raia Civil Rights, DHHS, JFK Federal Building Room 1875, Boston, MA 02203.

**Hutolipizwa kwa kutuma malalamiko. Misaada na huduma unazopata hazitohusishwa katika malalamiko yoyote unayotoa kwa afisa wa maswala nyeti wa AHS au kwa ofisi ya haki za jamii.**

**Ukiukaji wa ibara ya 42 CFR sehemu ya 2 (kuhusiana na sheria ya madawa na ulevi) ni uhalifu. Kukiwa na wasiwasi kwa kukiukwa kwa sheria hii unaweza kuripotiwa kwa Jaji Mkuu wa Marekani United States Attorney katika jimbo ambalo ukiukaji huo umetokea.**

Wakala wa Huduma za Jamii
Ilani ya mazoea ya faragha
Ilani hii inaanza kutumika kuanzia October 1, 2019

## USIRI WA HUDUMA KUHUSU: MAELEZO YANAYOMTAMBULISHA MTU

Pamoja na maelezo kuhusu usiri wa huduma zinazotolewa, AHS ina miongozo yanayohusu usiri wa maelezo yanayomtambulisha mtu ambaye tunampa misaada na huduma.

**Maelezo yanayomtambulisha mtu ni nini?**

. Haya ni maelezo yaliyopatikana au kupokelewa na AHS, au wakandarasi au wafadhili wao, ambayo yamamtambulisha au yanaweza kumtambulisha mtu anayepata huduma au misaada kutoka AHS. Mfano wa maelezo haya ni:

- Jina
- Namba ya ustawi wa jamii (Social Security)
- Tarehe ya kuzaliwa
- Anwani
- Namba ya simu

**Ni wakati gani AHS inatoa kwa wengine au kufichua maelezo yanayonitambulisha bila ya ruhusa yangu?**

Tunaweza kutoa kwa wengine au kufichua maelezo yanayokutambulisha kwa ajili ya mipango yetu ya kiutawala bila ya ruhusa yako. Mipango ya kiutawala ina maana shughuli muhimu katika kufanya kazi za AHS na zinahusu vitu vifuatavyo:

- Kuangalia maombi yako kama yanakubaliana na huduma na msaada uliyoomba, ikiwa pamoja na kutambua na kuratibu huduma hizi ndani ya AHS na wakandarasi na wadhamini wake.
- Kupanga, kugharamia na kufanya malipo kwa huduma na misaada inayotolewa kwa mtu na familia
- Uratibu wa misaada
- Kugundua wizi na matumizi mabaya
- Kuangalia kama sheria zinafuatwa na kuboresha shughuli zinazofanyika.
- Kwa dharura na wakati wa maafa
- Kufuata masharti ya kisheria ya Serikali kuu na Jimbo kwenye maswala ya kuripoti na mahitaji ya kifedha.

**Ni wakati gani AHS inahitaji ruhusa yangu kabla haijatoa kwa wengine na kufichua maelezo yangu yanayonitambulisha?**

Tunahitaji ruhusa yako kwa maandishi kuweza kutoa kwa wengine maelezo yako yanayokutambulisha ili:

- Kuangalia uwezekano wa kupata huduma zaidi ya zile ambazo umeshaziomba
- Kuwasiliana na watoa huduma kwako ambao hawana makubaliano au fedha kutoka kwetu.
- Kushauriana na wataalamu nje ya AHS ili kupata mawazo yao ya kitaalamu
- Kushauriana na wengine uliowachagua

Hatutoweza kutoa huduma tulizonazo kamili na kwa kiasi kinachotakiwa usipotoa ruhusa kwa sababu zilizotajwa hapo juu.

---

## Makubaliano

*Watoa huduma za moja kwa moja watafanya juhudi kupata ukubali wa mteja kupokea ilani hii. Kama mteja atakataakupokea, mhudumu ataandika taarifa juu ya juhudi iliyofanyika na sababu za mteja kukataa.*

Ninakubali kuwa nimepata nakala ya ilani hii.
Tarehe: ___________________________

_______________________________________________
(Sahihi yako au ya mwakilishi wako)